HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA

MPANGO MKAKATI WA UBORESHAJI MIUNDOMBINU YA MIFUGO, UTENGAJI MAENEO YA MALISHO NA UDHIBITI WA MIGOGORO YA WAFUGAJI NA WAKULIMA

UTANGULIZI

Wilaya ya Kilosa ina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 12,363.7 kati ya hizo eneo la malisho linakadiriwa kuwa ni hekta 430,000 na idadi ya watu ni 438,175 (Sensa 2012). Wilaya ina jumla ya Tarafa 7, Kata 40 na vijiji 139. Idadi ya wafugaji waliosajiliwa ni 6110 ambao idadi ya mifugo yao hadi sasa ni ng'ombe 155686, mbuzi 119481, kondoo 21953 na punda 2253. Hadi kufikia tarehe 22/10/2016 jumla ya ng'ombe 21993 wamepigwa chapa sawa na asilimia 14 ya ng'ombe waliosajiliwa. Zoezi la usajili limekumbana na changamoto ya mgomo katika baadhi ya maeneo ya Parakuyo, Godes, Kwambe, Mkundi, Kiduhi na Twatwatwa hivyo idadi kamili ya mifugo bado haijapatikana. Mpango wa uboreshaji wa miundombinu na huduma ya mifugo unalengo la kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Wilaya imeandaa mpango mikakati wa mwaka 2015 - 2020 ambao utahakikisha mazingira ya amani na usalama yanadumishwa ili mfugaji na mkulima na watumiaji wengine wa ardhi washiriki kikamilifu katika Shughuli za uzalishaji.

KUTAMBUA NJIA ZA KUPITISHA MIFUGO (STOCK ROUTES).

Halmashauri katika maeneo mbalimbali imebainishia njia za kupitisha mifugo ambazo zitasaidia kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Hadi sasa Halmashauri imebainisha njia za kupitisha mifugo (stock routes) zifuatazo;-

- Lumuma – Kilosa kwa mifugo inayotoka Mpwapwa (Dodoma),
- Malolo – Kisanga – Mfilisi – Mikumi kwa mifugo inayotoka Kilolo (Iringa),
- Mikumi – Kilombero kwa mifugo inayotoka Kilombero (Morogoro)
- Mtumbatu – Magubike – Dumila kwa mifugo inayotoka Gairo, Kongwa, na Kiteto.
- Kilosa – Mkata – Morogoro kwa mifugo inayoenda Morogoro
- Kilosa – Msowero – Dumila
- Kilosa – Ulaya - Mikumi

Pia Halmashauri imetoa maelekezo kwa Serikali za vijiji kusimamia wakulima kutoziba au kulima katika njia za kupitisha mifugo kwenda kunywesha katika vyanzo vya maji (mito na mabwawa).

MPANGO MKAKATI WA UBORESHAJI MIUNDOMBINU YA MIFUGO

Halmashauri kwa kushirikina na wadau mbalimbali wa maendeleo (World Vision, WARIDI, Wafugaji, TANAPA n.k) itaendelea kuboresha miundombinu ya mifugo Wilayani Kilosa. Hali ya miundombinu ya mifugo kwa sasa imeonyeshwa katika Jedwali lifuatalo:-

Miundombinu	Idadi jumla	Inayofanya kazi	Isiyofanya kazi	Inayohitaji ukarabati
Malambo	19	9	8	12
Majosho	23	6	11	17
Machinjio	5	4	-	2
Minada	6	5	1	4
Mabanda ya Ngozi	5	2	-	3
Vituo vya ukaguzi	1	1	-	-
Liv.holding ground	1	-	-	-
Makaro	16	16	-	16

1. Kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya mifugo

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imetenga fedha kutokana na vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha miundombinu mbalimbali ya mifugo kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali lifuatalo:-

MPANGO	KIJIJI	FEDHA ILIYOTENGWA		
		Mapato ya ndani	S/kuu	Wadau (ASDP, NGOs, Mashirika/ Wafugaji)
Kuchimba kisima kirefu cha maji, kufungwa pumpu na Ujenzi wa mabirika ya maji ya kunyweshea mifugo	Kiduhi	19,835,000	0	0
Ujenzi wa banda la ngozi na Uzio katika machinjio.	Masugu, Magomeni	30,000,000	48,000,000	0
Ujenzi wa karo la uchinjaji	Ilonga Msalabani	15,000,000	0	0
Ujenzi wa banda la ngozi na Uzio katika machinjio.	Kimamba	0	20,000,000	0
Ujenzi wa machinjio na banda la ngozi	Ruaha			200,170,000
JUMLA TSHS.		**64,835,000**	**68,000,000**	**200,170,000**

Halmashauri itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya majosho, malambo na uboeshaji wa nyanda za malisho na huduma za mifugo katika maeneo ya wafugaji ili kupunguza uhamaji holela wa mifugo Kutafuta maji na malisho.

2. Kutafuta wahisani na wadau mbalimbali wa maendeleo

Halmashauri imeendelea kuwashirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo (World Vision, WARIDI, Wafugaji, TANAPA n.k) katika kusaidia uboreshaji wa miundombinu ya mifugo

wilayani Kilosa. Katika kipindi cha mwaka mwaka 2014/2015 TANAPA (Mikumi) wamewezesha Uchimbaji wa malambo mawili ya mifugo katika kijiji cha Kiduhi.

Mradi wa WARIDI ambao unaojihusisha na uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali maji umeonyesha nia katika kusaidia upatikananaji wa maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo. Hatua za awali zimefanyika kubaini mahitaji ya visima virefu na Ujenzi wa mabirika ya kunyweshea mifugo pamoja na Uchimbaji wa malambo.

Halmashauri imefanya upembuzi yakinifu katika eneo la Mfilisi, Ihombwe na kuandaa mchoro wa lambo lenye ujazo wa 209,645m^3 kwa gharama ya Tshs. 595,800,800/- (BOQ, Januari 2014). Wahisani na wadau mbalimbali ikiwemo mradi wa WARIDI wameendelea kushirikishwa kuwezesha ujenzi wa mradi huu.

3. Kuwahamasisha wafugaji kuchangia uboreshaji wa miundombinu ya mifugo.

Halmashauri inaendelea kuhamasisha wafugaji kuchangia Shughuli za uboreshaji wa miundombinu ya mifugo kama vile malambo na majosho. Pia Halmashauri imewasilisana na Wizaza ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili kupata mwongozo na michoro ya malambo na majosho ya gharama nafuu ambayo wafugaji wataweza kumudu kuchangia Ujenzi.

MIKAKATI YA KUTENGA MAENEO YA MALISHO YA MIFUGO

1. **Kuandaa na kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi:** Halmashauri itaendelea kutenga maeneo ya malisho ambapo kila mwaka imejiwekea malengo ya kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 4.
2. **Kushirikisha wadau wa maendeleo:** Halmashauri imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile MKUHUMI, MKURABITA katika kupanga mpango ya matumizi bora ya ardhi. Jumla ya hekta 173,839 za malisho zimepimwa kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji 29 kama ilivyooneshwa katika **Kiambatanisho A.**
3. **Kuomba kufutwa kwa mashamba pori:** Halmashauri imeafanya ukaguzi na kutoa notisi ya mashamba pori 72 yenye ukubwa wa hekta 113,733.2. Kati ya haya mashamba 17 yenye ukubwa wa hekta 14486.3 mapendekezo ya kufutwa yamewasilishwa kwa Waziri wa Ardhi. Kufutwa kwa mashamba haya kutasaidia Halmashauri kuongeza eneo la malisho na kwa ajili ya Shughuli zingine.

4. **Halmashauri inapendekeza kufutwa kwa baadhi ya vitalu vya Mkata ranchi (NARCO) jumla ya hekta 12,000 ambazo hazijaendelezwa**: Vitalu hivyo vimekuwa chanzo cha migogoro kutokana na wawekezaji waliopewa kusindwa kuviendeleza kulingana na masharti, na kuwakodisha kwa wakulima hivyo kusababisha migogoro ya

mara kwa mara. Vitalu hivi wapewe wafugaji kwa ajili ya kuanzisha ranchi ndogo ndogo ili waweze kufuga kisasa.

MATUKIO YA MIGOGORO YA WAFUGAJI KULISHA MIFUGO YAO KWENYE MASHAMBA YA WAKULIMA

Katika kipindi cha mwezi Julai 2016, Halmashauri imepokea na kufanya tathmini jumla ya malalamiko 176 ya mifugo kuharibu mazao ya wakulima katika maeneo mbalimbali. Aidha kesi nyingi zimekuwa zikitatuliwa katika ngazi ya kijiji na kata kwa wafugaji kulipa fidia ya uharibifu wa mazao, hivyo malalamiko hayo kutofika Wilayani. Matukio yaliyoripotiwa Wilayani yameonyeshwa katika chati ifuatavyo:-



MIKAKATI YA KUDHIBITI MATUKIO YA WAFUGAJI KULISHA MIFUGO YAO KWENYE MASHAMBA YA WAKULIMA

i. **Kusajili wafugaji na kupiga chapa mifugo yao:-** mkakati huu utaiwezesha Halmashauri kudhiti uchungaji holela na kuwatambua wafugaji wavamizi. Zoezi la usajili mifugo na Upigaji chapa linaendelea na linatarajia kukamilika ifikapo tarehe 31/10/2016

ii. **Kufanya doria na ukaguzi wa kushitukiza:-** Mkakati huu umelenga kuwabaini wafugaji wavamizi kwa kufanya doria katika njia wanazozitumia na kuwaondoa kwa nguvu kuwarudisha walikotoka.

iii. **Kuondoa mifugo katika maeneo ya Kilimo na vyanzo maji:** - Katika kutekeleza mikakati Halmshauri kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya imeafanya ukaguzi wa kushitukiza na kuwaondoa wafugaji katika maeneo ya Kilimo kwenye kata za Mabwerebwere, Kilangali, Tindiga na Ulaya. Mfugaji Bw. Nyakungu ameaondolewa kwa amri ya Mahakama kwenye eneo la Kilimo katika kata ya Chanzuru.

Wafugaji watatu kutoka kata za Malangali, Zombo na Ulaya wamekamatwa na kufikishwa mahakamani na kufunguliwa kesi kwa makosa ya uchungaji holela katika maeneo ya Kilimo na kufanya uharibifu wa mazao.

iv. **Kuzuia uingizaji holela wa mifugo toka nje ya wilaya na kuzuia uchungaji holela wa mifugo ndani ya Wilaya.** Mkakati huu unazingatia Waraka wa Rais namba 1 wa mwaka 2002, Sheria ya Magonjwa ya Wanyama namba 17 ya mwaka 2003 pamoja na Vifungu namba 5 na 6 vya *Sheria ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya mwaka 2014* ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.

v. **Kamati ya Amani ya Wilaya imeundwa:** Kamati hii ina wajumbe kutoka Jamii za wafugaji na wakulima, Viongozi wa dini, Viongozi wa kimila, wazee maarufu, madiwani na Viongozi wa Chama na Serikali. Kamati imefanya vikao vitatu tarehe 22/08/2016, tarehe 14/09/2016 na tarehe 22/09/2016 na kuandaa hadidu za rejea na uchambuzi wa kina wa vyanzo vya migogoro na kutoa maoni yake. Maoni ya Kamati hii yatawasilishwa katika Kikao Maalum cha Menejimenti ya Halmashauri na Baraza Maalumu la Madiwani. Pia Kamati hii imetembelea Kijiji cha Madoto kutatua mgogoro wa ardhi na itapata fursa ya Kutembelea maeneo mengine yenye migogoro na kuzungumza na Jamii.

vi. **Kusimamia** ***Sheria ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya mwaka 2014*** ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kwa lengo la kuzuia uharibifu wa mazingira na kulinda misitu na vyanzo vya maji.

vii. **Kuanzisha vituo vya polisi katika maeneo yenye migogoro:** Kata ya Tindiga imetoa jengo na taratibu za kuweka kituo cha Polisi zinaendelea. Mhandisi ujenzi ameshaandaa ramani na makisio ya gharama za ujenzi wa kituo cha polisi **Tshs. 29,092,000/-** ambazo zitatokana na mchango ya Halmashauri, wadau mbalimbali na wananchi.

viii. **Kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria baadhi ya Viongozi na watendaji** ngazi ya kata/kijiji wasiowaaminifu ambao huwakaribisha wafugaji wavamizi katika maeneo yao.

ix. **Kuboresha sheria ndogo**: Halmashauri itafanya mapitio ya sheria ndogo za Halmashauri na ambazo ni Sheria ndogo ya Hifadhi Mazingira ya na Sheria ndogo ya Udhibiti wa uchungaji holela wa mifugo na kuzifanyia maboresho ili ziweze kuwa na kali zaidi kwa wafugaji wanaokiuka sheria.

HITIMISHO

Wilaya ina dhamira ya dhati katika kupunguza migogoro kati ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ili wananchi waishi kwa amani na kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji na kipato kujenga uchumi wa Taifa kwa ujumla. Halmashauri itaendelea

kutenga bajeti kila mwaka na kuwahamasisha wadau wengine wakiwemo wafugaji kuchangia kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu na huduma za mifugo.

Naomba Kuwasilisha,

Wako,

Kessy J. Mkambala
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
KILOSA

Kiambatanisho A:

Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Malisho Wilayani Kilosa

No.	**Kata**	**Kijiji/eneo**	**Eneo la malisho** (ha)
1	Parakuyo	Parakuyo	30830
2	Parakuyo	Ngaite	34580
3	Kilangali	Kiduhi	24270
4	Dumila	Kwambe	12000
5	Kitete	Mabwegere	10232
6	Msowero	Msowero GODES	7200
7	Madoto	Mbwade	7200
8	Mikumi	Ihombwe (Mfilisi)	34704
9	Berega	Berega	432
10	Magubike	Magubike	364.418
11	Kilangali	Kivungu	-
12	Masanze	Changarawe	-
13	Masanze	Dodoma-Isanga	114.75
14	Masanze	Lunenzi	950.75
15	Malolo	Malolo A	1094.8
16	Mabwerebwere	Malangali	-
17	Ruaha	Ruaha	504.28
18	Mvumi	Mvumi	2224
19	Mhenda	Mhenda	600
20	Mhenda	Kitunduweta	222.5
21	Ulaya	U/mbuyuni	44.5
22	Ulaya	U/kibaoni	472
23	Zombo	Kigunga	132.04
24	Zombo	Nyali	156.23
25	Kisanga	Kisanga	246.03
26	Chanzuru	Mfuluni	325.25
27	Chanzuru	Idete	208.075
28	Lumbiji	Kisongwe	3836.15
29	Maguha	Maguha	895.625
	Jumla ya Eneo la Malisho (hekta)		**173,839.398**